

ecoagriculture
Mwelekeo wa Sera
No.11 Oktoba 2014

# Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji: Mbinu ya mapinduzi ya kijani wilayani Mbarali, Mbeya

## Muhtasari

*Nchini Tanzania, mpango wa matumizi bora ya ardhi vijijini ulirasimishwa miaka ya hivi karibuni ikiwa ni moja ya mikakati katika mchakato wa kuleta maendeleo endelevu vijijini. Utekelezaji wa mpango huu hauna budi kuwa mikononi mwa wanavijiji wenyewe kwa kiasi kikubwa katika kugawa ardhi yao kwa matumizi mbalimbali ya kujikimu kimaisha kwa sasa na siku za baadaye na kuwa na uhifadhi endelevu wa mazingira. Maendeleo endelevu katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya yanaathiriwa na migogoro ya matumizi ya rasilimali ardhi na maji kwa muda mrefu sasa. Hii imetokana na uwezo wa ardhi kupungua kutoa mavuno ya kutosha na uhaba wa maji kwa matumizi mbalimbali hususan umwagiliaji, unyweshaji mifugo, uendelevu wa miminiko la maji kwenye bwawa la umeme, uhifadhi ya bionuai na mazingira. Mpango wa matumizi bora ya ardhi vijijini unasaidia kusimamia na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi, maji na hifadhi ya mazingira. Tafiti katika kijiji cha Mabadaga chenye mpango rasmi wa matumizi bora ya ardhi na kijiji cha Matebete chenye mpango usiorasmi wa matumizi bora ya ardhi zinaonesha kupungua kwa migogoro kati ya watumiaji ardhi ndani ya vijiji na uhifadhi wa mazingira umeboreka kutokana na kuwa na mpango. Ushuhuda toka kwa viongozi na wanavijiji unathibitisha kuwa, kuna ongezeko la kutiririka kwa maji kutoka kwenye vyanzo, kurejea kwa uoto wa asili na wanyama pori katika maeneo yaliyotengwa kuwa hifadhi ya misitu. Pia, migogoro yatokanayo na mifugo kuharibu mazao yameweza kusimamiwa na kusuluhishwa kwa kuzingatia sheria na taratibu au maelewano yaliyowekwa na jamii katika vijiji hivyo. Pamoja na hayo, mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji unawawezesha, wakulima kuomba na kupewa haki miliki ya ardhi ya kimila. Ingawa wafugaji, bado hawaoni suala la haki miliki ya kimila ni muhimu kwao kwa hivi sasa kwa kuwa maeneo yaliyotengwa kwa malisho ni ya wote. Utafiti umebainisha kuwa maslahi ya jamii ya waliowachache katika kijiji hususan wafugaji yasipozingatiwa wakati wa kuandaa mpango, migogoro haitaweza kusimamiwa kikamilifu hasa wakati wa kiangazi, ambapo uhaba mkubwa wa malisho na maji unakuwepo.*

*Utafiti huu umebaini kuwa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji, hauwasadii wanakijiji kusuluhisha migogoro ya mipaka baina ya vijiji, kwa kuwa suala la mipaka ya vijiji iko nje ya mamlaka ya serikali za vijiji. Pia, imefahamika kuwa migogoro ya mipaka baina ya vijiji hukwamisha utekelezaji wa sera ya vijiji kuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi. Hivyo, hakuna budi mamlaka husika katika ngazi ya wilaya kuweka utaratibu wa kutatua migogoro ya mipaka kati ya vijiji ili kuharakisha maendeleo endelevu na mapinduzi ya kijani kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi.*

## Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua umuhimu wa kilimo cha wakulima wadogo kuwa ni mhimili wa uchumi wa Taifa. Zaidi ya asilimia 80 ya watanzania wameajiriwa na shughuli za kilimo, ambayo zinawapa chakula na kipato cha kujikimu kimaisha. Hivyo, kilimo ni msingi wa maendeleo endelevu nchini hasa katika kuwa na uhakika wa chakula na kupunguza umaskini. Pamoja na mchango wa moja kwa kwa moja katika maisha ya wananchi, kilimo huchangia robo au asilimia 25 ya pato la taifa (SAGCOT, 2011). Kutokana na mchango huu mkubwa wa kilimo na fursa ya rasilimali ardhi iliyopo kwa ustawi wa wananchi na uchumi wa Taifa, serikali imetoa kipaumbele katika kilimo. Hivi karibuni, serikali imetoa msukumo wa pekee wa kuongeza uzalishaji kwa kuwa na



*Afisa Mipango Wilaya ya Mbarali, Geoffrey Mwaijobele akiwa na watafiti wakipitia ramani za vijiji, Wilayani Mbarali. Picha imepigwa na: Abigail Hart*

mikakati ya uwekezaji katika kilimo wa sekta za umma na binafsi kupitia mikakati maalum ya *Kilimo Kwanza* na *Matokeo Makubwa Sasa*.

Nyanda za Juu Kusini ni eneo lenye mvuto mkubwa kutokana na maslahi mbali mbali inayotokana na fursa za utajiri wake wa asili, hususan viumbe hai, kuwa chanzo cha maji kwa ajili ya umeme na umwagiliaji, kuwa na hifadhi ya wanyama pori na mazingira mazuri. Mvuto huu unasaidia kupanuka kwa fursa za maendeleo na kiuchumi katika Kanda. Ingawa sera zinatamka wazi na kwa msisitizo kuwa uwekezaji unalenga ustawi wa wakulima wadogo wadogo nchini, baadhi ya wadau wamehoji kama utekelezaji wa mikakati hiyo utawanufaisha wakulima wadogo katika maendeleo ya kiuchumi au la.

Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji (MMaBAVi) ni moja ya mipango mkakati ya utekelezaji utakaohakikisha wakulima wadongo na wafugaji wananufaika na sera ya uwekezaji katika ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi nchini. Sheria ya ardhi ya kijiji ya Namba 5 ya Mwaka 1999, ni mojawapo ya miongozo yanayoelekeza utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi vijijini. Sheria hii inaipa mamlaka na maelekezo serikali za wilaya kusimamia mchakato utakaoshirikisha wananchi vijijini kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi yao. Utekelezaji mzuri, utakaozingatia sheria unatarajiwa kupunguza migogoro yanayotokana na matumizi ya ardhi na mali asili nyingine zilizopo katika kijiji. Mpango wa matumizi bora ya ardhi unaweka utaratibu wa kisheria wa wananchi kugawa ardhi yao katika matumizi mbali mbali, ikiwemo kilimo, mifugo, makazi, hifadhi ya misitu na vyanzo vya maji, uwekezaji n.k. Utaratibu huu unatarajiwa kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi na maliasili nyingine na unaweka utaratibu wa kisheria unaomwezesha kila mwananchi kupata hati miliki ya kimila ya ardhi yake. Mpango mkakati huu ni hatua muhimu, si lengo la mwisho ili kufikia maendeleo ya kiuchumi.

Wadau tofauti wa maendeleo wameonesha kuvutiwa na MMaBAVi ili kufanikisha malengo yao tofauti ya kimaendeleo yakiwemo: uhakika wa kuwa na miliki ya ardhi kwa wananchi vijijini, kutenga mapito kati ya hifadhi za wanyama pori, fursa ya maendeleo ya kiuchumi kwa kuzingatia hifadhi ya misitu na mazingira, kuhamasisha uwekezaji mkubwa n.k. Mkoani Mbeya, viongozi katika fani za kilimo na hifadhi wanaona mpango mkakati wa matumizi bora ya ardhi ni fursa muhimu ya mapinduzi ya kijani kwa kuzingatia hifadhi ya mali asili na bionuai, ili kuwa na kilimo endelevu chenye tija kwa wakulima na wafugaji katika maeneo yao.

## Mchakato na Malengo

Nchini Tanzania, tafiti na zoefu za MMaBAVi kutoka mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ni haba, baadhi ya zilizopo ni

*Mmoja wa watafiti akifanya mahojiano na mwanakijiji wa Matebete . Picha imepigwa na: Abigail Hart*



kutoka Mikoa ya Kanda ya Kaskazini. Kutokana na ukweli kwamba mvuto wa wadau wa maendeleo kuwekeza mikoa ya Nyanda za Juu Kusini unaongezeka kwa kasi, ni muhimu kutathmini utekelezaji wa MMaBAVi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Malengo ni kutathmini ufanisi, mafanikio na mapungufu katika mchakato wa utekelezaji wa mpango, ili kuweza kushauri halmashauri ya wilaya na wadau wa maendeleo kufanya maboresho yatakayoleta ufanisi na mafanikio ya kuwa na mabadiliko ya kijani na maendeleo endelevu.

Matokeo haya ya awali na mapendekezo yametokana na tafiti na zoefu toka vijiji vitatu, wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya. Malengo mahususi ya utafiti huu ni: (1) kutathmini kiwango na ufanisi katika utekelezaji wa MMaBAVi katika vijiji vya wilaya ya mbarali; (2) kubaini namna ambavyo mpango unachangia katika malengo ya maendeleo ya wanavijiji, kama vile kuongeza uhakika wa miliki ya ardhi kwa matumizi mbali mbali ya wakulima na wafugaji; na (3) kubaini kiwango cha ushirikishwaji wa wanavijiji na wadau wengine, hususan masuala ambayo wangependa yazingatiwe katika mchakato wa kuandaa MMaBAVi vyao.

Ili kupata yaliyokusudiwa kwenye malengo hayo, mchakato ulikuwa kufanya mazungumzo na viongozi wa ngazi ya wilaya na vijiji na wananchi wenyewe katika vijiji vitatu vya mabadaga, maluma na matebete wilayani mbarali. Mazungumzo yalijikita kwenye ufanisi, mafanikio na mapungufu ya mchakato wa utekelezaji wa sera ya mpango wa MMaBAVi. Watafiti walitumia mbinu za kudodosa namna ambavyo MMaBAVi ulichangia au kutochangia kwenye malengo yao ya maendeleo, uelewa na ushiriki wa wanavijiji katika hatua za mchakato wa utekelezaji na kuridhika/kutoridhika na matokeo ya mchakato wa utekelezaji wa MMaBAVi.

Mazungumzo yalijikita kuelewa mazingira ya kisera yatakayowezesha kuboresha utekelezaji wa MMaBAVi kwa ufanisi na mafanikio katika mkoa wa Mbeya. Kuelewa mazingira hayo yatasaidia wadau wa maendeleo kufahamu namna watakavyoshiriki katika mchakato wa MMaBAVi na changamoto zilizopo kufanikisha na uwekezaji katika kilimo kinachosaidia maendeleo ya wakulima na wafugaji wadogo kuwa na uzalishaji endelevu na wa tija ya juu.

## Yaliyobainika

### *Mafanikio na Faida ya MMaBAVi*

***Ushirikishwaji wa wananchi*** - Utafiti umebaini kuwa wananchi wote walishirikishwa vyema katika hatua za mchakato kama zilivyoainishwa na kuelekezwa katika itifaki ya Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi. Katika vijiji vilivyotembelewa vyenye MMaBAVi, makundi yote ya wadau katika vijiji hivyo vimeshirikishwa na kukiri ushiriki wao, hata pale ambapo kumekuwa na baadhi yao kutoridhishwa na maamuzi yaliyojiri kutokana na mchakato.

***Kutengwa maeneo ya hifadhi yanayosimamiwa na wananchi*** - Kutengwa kwa maeneo ya hifadhi yanayosimamiwa na wananchi wenyewe katika utekelezaji wa MMaBAVi, imedhihirika kuwa jamii katika vijiji hivyo inaheshimu mipaka na sheria ndogo ndogo inayosimamia matumizi ya maeneo hayo. Katika baadhi ya vijiji tayari maeneo hayo yaliyotengwa kwa hifadhi yameanza kuleta matokeo tarajiwa,yakiwemo kurejea kwa mito na vijito vinavyotiririsha maji na kurejea kwa wanyama pori na uvunaji endelevu wa miti kwa mahitaji ya kaya za wanavijiji. Pia, maeneo hayo yameanza kuwa fursa za shughuli mpya za kiuchumi kwa wananchi, hususan, ufugaji wa nyuki.

***Utatuzi wa Migogoro*** - Kwa kuwa MMaBAVi inaweka mipaka, sheria ndogo ndogo na utaratibu wa usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kijiji, hurahisisha maamuzi ya utatuzi wa migogoro baina ya makundi ya watumiaji ndani ya kijiji. Hivyo, MMaBAVi imekuwa chombo cha kusimamia rasilimali na kuharakisha utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi na rasilimali nyingine katika vijiji vyenye nayo. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa MMaBAVi haisadii katika kusuluhisha migogoro ya mipaka baina ya vijiji. Ni sharti kuwa, kabla ya vijiji kuandaa MMaBAVi migogoro ya mipaka baina ya vijiji ni lazima kutatuliwa kwanza.

***Uhakika wa Miliki ya Ardhi*** - Kuwa na MMaBAVi, haiwahakikishii wakulima kuwa na usalama katika uhakika wa miliki ya ardhi. Hata hivyo, ili kupata haki miliki ya ardhi ya kimila iwapo kijiji kina

*Mmoja wa wanakamati ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya kijiji na mmoja wa wafugaji wakibadilishana uzoefu katika kijiji cha Mabadaga. Picha imepigwa na: Abigail Hart*



MMaBAVi mchakato wa kutoa unakuwa rahisi kwa wakulima na wafugaji.

## Mapungufu Katika Mchakato wa Kuandaa MMaBAVi

***Elimu ya Mchakato wa Kuandaa MMABAVi*** -Viongozi wa halmashauri za vijiji na wanavijiji wengi wamesikia kuhusu sheria Namba 5 ya ardhi ya vijiji ya mwaka 1999 na kuhusu MMaBAVi. Hata hivyo, uelewa wa hatua zinazotakiwa kufuatwa katika maandalizi ya MMaBAVi ni mdogo kwa wengi. Tathmini imeonesha kuwa ni wachache sana wanaoelewa hatua za kuandaa MMaBAVi na bajeti inayohitajika kwa kazi hiyo.

***Kukosekana kwa Mipango ya Baadaye Katika MMaBAVi*** - Mipango ya sasa haikuweza kuzingatia kutenga maeneo kwa matumizi ya uwekezaji na ongezeko la idadi ya watu, ambayo huenda yakaleta mabadiliko ya matumizi kadiri idadi ya watu inavyoongezeka.

***Mgawanyo wa Rasilimali Usiowiana*** - Pamoja na ushirikishwaji wa wote katika mchakato wa kuandaa MMaBAVi, mgawanyo uliopo umerasimisha sheria na kanuni zinazokwamisha wakati mwingine kuwa na fursa ya matumizi ya rasilimali, kama vile maji kwa kundi la jamii moja kwenye kijiji. Kwa mfano mapito ya mifugo ya wafugaji kwenda kunywesha maji na/au maeneo yenye malisho wakati wa kiangazi. Mgawanyo wa aina hii unaendeleza kutokea kwa migogoro baina ya makundi ya jamii tofauti. Hii inakuwa tatizo, kwa jamii husika pale viongozi wa kijiji wanapokaribisha wahamiaji kwa njia za kujinufaisha wao binafsi bila kujali athari ya kupungua kwa eneo au rasilimali kwa jamii iliyopewa ardhi hiyo awali.

## Changamoto

Ingawa kuwa na MMaBAVi, ni fursa ya kupata haki miliki ya ardhi ya kimila kwa wanavijiji, bado kuna changamoto zinazokwaza utekelezaji wilayani mbarali. Chanagmoto kuu mbili za utekelezaji wa MMaBAVi, wilayani Mbarali ni kama ifuatavyo:

Kwanza, ni kikwazo cha bajeti ambayo inafanya utekelezaji usiwe wa ufanisi na kasi katika wilaya. Bajeti ya kuandaa MMaBAVi, ni kidogo kiasi cha kutosha tu kijiji kimoja au viwili kwa mwaka. Vijiji vyenye MMaBAVi mpaka sasa ni 26 kati ya 99 wilayani Mbarali. Wilayani Mbarali kuandaa MMaBAVi katika kijiji kimoja inagharimu shillingi milioni 6-8. Kwa sasa, kutokana na hali ya upungufu mkubwa wa bajeti, MMaBAVi katika vijiji vingine vilitekelezwa kwa kutegemea wafadhili au kwa michango ya wanavijiji wenyewe.

Pili, ingawa baadhi ya vijiji vimekuwa na mafanikio kwa kuweza kuendeleza MMaBAVi kutokana na msaada mdogo kutoka ngazi ya halmashauri ya wilaya, vijiji vingine vimekuwa na vikwazo katika mchakato wa kukamilisha utekelezaji. Vijiji vichache vimeweza kuchanga kiasi cha fedha ili kuandaa MMaBAVi vyao, lakini uelewa na kukosa uwezeshwaji katika hatua za kufuata



*Picha imepigwa na: Abigail Hart*

umekwamisha jitihada zao,wanahitaji kusaidiwa kupiga hatua katika mchakato wa utekelezaji ili kufikia malengo.

Katika changamoto hizi, wadau wengine wa maendeleo wanasadia, hususan, mashirika yasiyo ya serikali katika utekelezaji MMaBAVi. Mashirika hayo yameweza kusukuma na kusadia katika hatua ambazo vijiji vinakwama kuendelea na maandalizi ya MMaBAVi na pia katika mchakato wa wilaya kupitisha haraka sheria ndogondogo ya kusimamia maeneo yaliyotengwa kwa makusudi maalum. Badhi ya wadau walisadia utekelezaji wa MMaBAVi, kufikia malengo yao (Jedwali Na 1). Kwa sasa bado hakuna juhudi za makusudi ya kuelewa kwa undani vichocheo na tofauti ya wadau yanayosadia kuandaa MMaBAVi. Kuelewa bila kuzipuuza vichocheo na tofauti zao kwa umakini ni hatua mojawapo ya kufikia malengo mapana ya kufanikisha matokeo makubwa katika kuwa na kilimo endelevu na ya tija inayozingatia hifadhi ya viumbe hai tofauti (bionuai) na mazingira kwa ujumla.

## Hitimisho na Mapendekezo

**1** Umuhimu na motisha ya kuwa na MMaBAVi umeeleweka vizuri kwa wakulima. Wanaona inawawezesha kupata haki miliki ya kimila ya ardhi ambayo inaongeza thamani ya ardhi yao, kuwa na urahisi wa kupata mikopo ya kuwekeza kwenye kilimo na uwezo wa kisheria wa kulinda rasilimali ardhi. Pia, MMaBAVi vinazuia kilimo cha kuhamahama inayoharibu bionuai na mazingira, badala yake wakulima wanawekeza katika mbinu za kilimo bora na endelevu kuongeza uzalishaji katika maeneo waliyonayo.

**2** Katika kilimo cha mazao, shughuli za huduma za ughani zikiwemo upatikanaji wa pembejeo, huduma za ushauri na elimu za mbinu bora na endelevu kuongeza uzalishaji wa mazao imewafikia wakulima. Hata hivyo, kwa upande wa kilimo cha mifugo huduma za ughani wa mbinu za uzalishaji, pembejeo na elimu bado ni haba ili kuwa na ufugaji bora na endelevu. Ni lazima kwa halmashauri kutambua kuwashirikisha kikamilifu wafugaji katika kuandaa MMaBAVi, kuwa na mkakati wa huduma za ughani kama pembejeo, elimu na mbinu za kuboresha mifugo na maeneo ya malisho. Hii ni muhimu kuhakikisha kuwa na tija na uendelevu katika ufugaji na hifadhi ya mazingira.

*Jedwali Na. 1. Wadau walioshiriki katika maandalizi ya MMaBAVi Wilayani Mbarali, michnago yao katika malengo ya muda mrefu ya kuongeza tija na kuwa na kilimo endelevu.*

| Mdau | Malengo | Michango kwenye malengo ya muda mrefu kuongeza tija na kilimo endelevu |
|---|---|---|
| Serikali ya wilaya | Kusimamia na utatuzi wa migogoro, uhifadhi na uwekezaji | • Kuhakikisha kwamba MMaBAVi kuchangia kwenye taswira ya maono ya wilaya na mipango ya uhifadhi na uwekezaji kuwa na maisha bora ya watu na uendelevu katika matumizi ya rasirimali ya asili |
| Viongozi wa vijiji | Kusimamia na utatuzi wa migogoro, kuwa na maendeleo ya kiuchumi | • Kuainisha maeneo ya hifadhi ndani ya kijiji<br>• Kutoa elimu na vitini vya ushauri wa mbinu za uzalishaji endelevu wa kilimo cha mazao na ufugaji<br>• Kujenga na kuimarisha mahusiano na mashirika yenye utalaam wa maendeleo ya jamii kusaidia kuwajengea wananchi uwezo |
| Wakulima na wafugaji | Uhakika wa kuwa na haki miliki ya ardhi, kupata mitaji, upatikanaji wa maji na fursa ya kutumia rasilimali za asili kwa shughuli za kiuchumi. | • Kutumia mbinu za kilimo na ufugaji bora katika maeneo/mashamba ya kila mmoja<br>• Fursa ya upatikanaji wa mitaji ya kuwawezesha kupata pembejeo na huduma nyingine za ughani katika kuendesha kilimo na ufugaji bora kwa mbinu endelevu.<br>• Kuanzisha na/au kuimarisha vikundi au umoja au vyama kwa wakulima na wafugaji kuwawezesha kubadilishana maarifa na zoefu za mbinu za kilimo na ufugaji endelevu |
| Mashirika ya uwezeshaji jamii na mipango ya maendeleo serikalini | Kuwa na maeneo makubwa ya hifadhi ya rasilimali asili (bionuai na mazingira), kuwa na uwekezaji katika mashamba makubwa, urasimishaji wa ardhi na umiliki wa biashara n.k | • Kuwa na miongozo na itifaki kwa ajili ya uwekezaji endelevu<br>• Kuelimisha jamii kuhusu fursa na thamani zinazotokana na hifadhi ya bionuai na uboreshaji endelevu wa kilimo na rasilimali za asili<br>• Kuwezesha upatikanaji wa masoko kwa vikundi, umoja au vyema vya wakulima na wafugaji wadogowadogo na kuwa na fursa za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo ili kuongeza faida na wananchi wengi kushiriki shughuli za maendeleo na za kiuchumi<br>• Kutoa ushauri kwa serikali ya wilaya kuhusu maeneo yanayofaa kuwa hifadhi na kwa uwekezaji, ama kuwa fursa za shughuli nyingine za maendeleo ya kiuchumi<br>• Kutoa fedha na uwezeshaji wa kitaaluma katika kuandaa MMaBAVi |

**3** Inaonekeana kuwa uzoefu wa utekelezaji wa MMaBAVi wilayani Mbarali bado ni mdogo, ni asilimia 26 tu ya vijiji katika wilaya. Tunapendekeza kwamba kabla ya kuendelea na maandalizi ya MMaBAVi katika vijiji vilivyobakia, ni vyema kwa wilaya kutathmini zoefu za utekelezaji toka vijiji vilivyo na MMaBAVi sasa ili kubaini kama utaratibu ulifuatwa, jamii inaridhishwa na MMaBAVi na jinsi inavyokidhi mabadiliko ya mahitaji mapya ya matumizi ya ardhi ya vijiji. Zoefu toka vijiji venye MMaBAVi zitaisaidia wilaya kutekeleza mpango kwa ufanisi na mafanikio zaidi katika vijiji vilivyobakia katika wilaya. Pia, wilaya inaweza kubaini kama vijiji vinazingatia sheria na miongozo ya utekelezaji wa MMaBAVi na kuchukua hatua kwa wakati muafaka kufanikisha utekelezaji na malengo.

**4** Utekelezaji wa MMaBAVi ni muhimu kufanikisha malengo ya wadau wengi wa maendeleo wa Nyanda za Juu Kusini. Malengo hayo ya wadau ni muhimu katika kusaidia utekelezaji wa haraka, hivyo yanapaswa kutambuliwa kuwa ni fursa na kuwekewa mazingira ya kusadia katika kuharakisha utekelezaji wa MMaBAVi katika Kanda. Wanavijiji wengi kutoelewa sheria na mchakato wa utekelezaji mzuri wa MMaBAVi, ni changamoto kwa wilaya na wadau wa maendeleo. Kukabili changamoto hizo wilaya kwa kushirikiana na wadau, ni lazima kuandaa na kusambaza vitini katika vijiji vyote vya wilaya. Vitini hivyo, vieleze kwa ufasaha mchakato wa kuandaa MMaBAVi, gharama za msingi zinazohitajika na ushiriki wa wadau katika mchakato.

**5** Kutokuwa na migogoro ya mipaka baina ya vijiji vinavyo pakana ni sharti muhimu kwa kijiji kuruhusiwa na kuanza machakato wa kuandaa MMaBAVi. Hivyo, migogoro ya mipaka baina ya ardhi za vijiji ni moja ya vikwazo vinavyosababisha utekelezaji wa MMaBAVi katika baadhi ya vijiji pamoja na wananchi kuchangia gharama. Usimamizi na utatuzi wa migogoro ya mipaka baina ya vijiji ni suala la kisheria na jukumu ambalo liko nje ya mamlaka ya serikali za vijiji husika. Ni lazima halmashauri ya wilaya kwa kushirikiana na serikali za vijiji, kusaidia katika kuweka taratibu za kufafanua na kuweka mipaka baina ya vijiji vyenye migogoro, ili kuharakisha mchakato wa utekelezaji wa MMaBAVi katika wilaya.

**6** Pamoja na kuwa kuna ushirikishwaji wa jamii katika mchakato wa utekelezaji wa MMaBAVi, imethibitika kuwa mahitaji ya makundi ya walio wachache hayapati nafasi ya kuzingatiwa. Ili kufanikiwa katika malengo ya kusimamia na kutatua migogoro kwa kiasi cha kuridhisha baina ya wanakijiji, mchakato wa utekelezaji wa MMaBAVi unahitaji kutia maanani mahitaji ya makundi ya wachache ambayo itazingatiwa katika kutenga matumizi ya rasilimali ardhi ndani ya kijiji.

**7** Kwa malengo ya maendeleo endelevu, ni muhimu wilaya kwa kushirikiana na vijiji kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi ya wilaya. Mpango huo utenge wilaya katika maeneo ya hifadhi ya misitu na vyanzo vya maji, kilimo, malisho ya mifugo wakati wa masika na kiangazi na maeneo ya uwekezaji. Mpango

wa wilaya uzingatie maeneo ya akiba kwa malengo ya muda mrefu kutokana na ongezeko la watu na mahitaji ya maendeleo ya kiuchumi. Kwa kutumia mpango huo wilaya itakuwa katika nafasi nzuri kuvishauri vijiji mtazamo wake madhubuti wa kuelekea kwenye maendeleo endelevu, hususan, kiuchumi, kijamii na uhifadhi wa mazingira. Kwa kuwa na mpango huo wilaya itajiwekea hazina ya mahusiano ya muda mrefu na wadau wa maendeleo katika kusaidia kuweka mikakati endelevu na utekelezaji wa mtazamo wake.

## Shukurani:

Timu hii ya watafiti inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mbarali kwa kutupa ruhusa ya kufanya utafiti katika wilaya yake. Shukrani za pekee ni kwa Bw Geofrey Mwaijobole, Afisa Mipango Miji wa Wilaya kwa kusaidia kutupa maelezo ya kina na taarifa za utekelezaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi yanayoendelea wilayani Mbarali. Tunawashukuru Watendaji na Wananchi wa Vijiji vya Madabaga, Mwaluma na Matebete kwa muda na ushirikiano wakati wa utafiti huu. Shukrani za pekee ziwaendee watafiti wasaidizi kwa kusaidia katika kupata takwimu na katika kusadia kuzichambua kuandaa taarifa hii.

Shukrani maalum ni kwa Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Kilimo Uyole, kwa kusaidia maandalizi na nyenzo za kutekeleza utafiti huu. Taasisi ya kimataifa ya wadau wa Ardhi (International Land Coalition), Hivos and Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD) zimefadhili utafiti huu.

## Imeadaliwa na:

Abigail Hart, Chuo kikuu cha Cornell na Taasisi ya Washirika wa EcoAgriculture

Elly Tumsifu, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam

Winnie Nguni, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam

John Recha, ERMCSD

Zacharia Malley, Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Kilimo-Uyole

Rodgers Masha, Mwakilishi wa Washirika wa Kilimo Tanzania

Louise Buck, Chuo kikuu cha Cornell na Taasisi ya Washirika wa EcoAgriculture

## Makala Mengine ya Kusoma:

**Hart, A.K., E. Tumsifu, J. Recha, W. Nguni, Z. Malley, R. Masha and L. Buck. 2014.** Participatory land use planning to support Tanzania farmer and pastoralist investment in green growth: Experiences from Mbarali District, Mbeya Region, Tanzania. Washinton, DC: EcoAgriculture Partners.

**Milder, J. C., L. E. Buck, A. K. Hart, S. J. Scherr, and S. A. Shames. 2013.** A framework for Agriculture Green Growth : Greenprint for the Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT). SAGCOT Centre, Dar es Salaam.

**United Republic of Tanzania (URT). 1999.** Village Land Act No. 5. Dar es Salaam: Government Printer.

### Mwelekeo wa Sera

Mfululizo wa machapisho yanayo lenga sera ya Kilimo-Mazingira (EcoAgriculture), imeandaliwa na washirika wa Kilimo-Mazingira kwa kushirikiana na mashirika mengine, katika masuala muhimu kwa wataalamu wa sera na wafanya maamuzi katika kilimo na hifadhi ya mazingira ili kuleta tatuzi husishi ya vikwazo vya maendeleo ya watu vijijini.

Kazi hii imefadhiliwa na ILC, maoni yanayoainishwa hapa yanaonesha mpangilio wa mwandishi na kwa vyovyote vile yasichukuliwe kama kiashirio/mtazamo rasmi cha ILC (International Land Coalition's initiative on Family Farming and People-Centred Land Governance).

INTERNATIONAL LAND COALITION

ecoagriculturepartners ERMCSD